**TAARIFA YA KUKAMATWA KWA WAKILI YONAS MASIAYA NA KUNYIMWA DHAMANA KATIKA KITUO CHA POLISI KATI ARUSHA**

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) unalaani kitendo cha cha Jeshi la Polisi kumkamata na kumnyima dhamana wakili Yonas Masiaya tangu jana Aprili 30, 2024. Wakili Masiaya alikamatwa jana jioni kwa tuhuma za kusambaza picha ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha kwenye makundi ya WhatsApp. Baada ya kukamatwa wakili Masiaya alinyang'anywa simu yake na kupelekwa katika kituo cha Polisi kati Arusha.

Licha ya kwamba tuhuma zinazomkabili wakili Masiaya zinadhaminika lakini Polisi walimnyima dhamana wakili huyo kwa madai kuwa wanasubili maelekezo kutoka juu. Leo Mei Mosi 2024 wakili Ngeeyan Oloibormunyei Laizer pamoja na familia ya wakili Masiaya walifika katika kituo cha Polisi kati Arusha kufuatilia dhamana yake lakini Polisi hawajatoa dhamana hiyo kwa wakili Masiaya wakidai kuwa wanasubili maelekezo kutoka juu.

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) umewaelekeza mawakili wake mkoani Arusha kufuatilia suala hilo kwa ukaribu pamoja na kuandaa nyaraka kwaajili ya kufungua kesi dhidi ya Jeshi la Polisi kwa kumshikilia wakili Masiaya bila ya kumpa dhamana kwa tuhuma ambazo hata yeye mwenyewe angeweza kujidhamini. Lakini pia THRDC inaamini kwamba Mkuu wa Mkoa ni mtumishi wa umma, hivyo picha yake kusambazwa kwenye makundi ya WhatsApp ni jambo la kawaida.

**Wito wetu**

- Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) unatoa wito kwa Jeshi la Polisi kumuachia wakili Masiaya kwa dhamana.
- Mtandao unatoa wito kwa jeshi la Polisi kufanya upelelezi kwa kuzingatia Sheria na Amri Kuu za Jeshi la Polisi (PGO). Jeshi la Polisi halipaswi kufanya kazi kwa kusubili maelekezo kutoka juu ambayo ni nje ya utaratibu wa kisheria.
- Kama kweli kuna tuhuma zinazomkabili wakili Masiaya, Polisi walipaswa kufanya upelelezi kabla ya kumkamata wakili Masiaya.
- Bado tunaendelea kudai mabadiliko ya sheria ya makosa ya kimtandao kwani imegeuka kuwa shubiri na kutumika vibaya kukamata na kubinya uhuru wa watanzanaia kutumia mitandao kukosoa, kuhoji na kutetea haki za binadamu. Sheria hii inachangamoto nyingi ikiwemo kuwapa Polisi mamlaka ya kuchukua vifaa vya mawasiliano vya watuhumiwa na kuingilia faragha zao kinyume na Sheria za ulinzi wa taarifa na faragha.

**Imetolewa na,**

**Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC),**

**Mei 01, 2024 Dar es Salaam, Tanzania.**